


Hapo zamani za kale, palikuwa na paka watatu walioishi pamoja. Paka mweusi, Paka wa bluu na Paka wa kijani.



Kila baada ya kula chakula cha jioni, paka wa bluu alioka mikate mitatu.

Kila walipoamka asubuhi, walikaa mezani wakapata kifungua kinywa chao cha mikate, maziwa na supu.



Asubuhi moja hawakuukuta
mkate mmoja, hivyo waligawana
mikate miwili tu.





Siku iliyofuata mkate mmoja ulitoweka tena. Walijiuliza wenyewe, "sasa tutafanyaje? Tutawezaje kumpata mwizi wetu?"



Paka  mweusi aliwaambia wenzake, walinde kwa zamu, kila mmoja awe na zamu ya siku ya kulinda usiku.



Kwa kuwa walikuwa wakila na kushiba kabla ya kulinda, kila mmoja alikuwa anapitiwa na usingizi bila kulinda.



Hata walipoamua kulinda kwa pamoja, pia walipitiwa na usingizi.

Haikuwa rahisi kumjua mwizi wao, hali hii iliendelea na kundelea.



Siku moja Paka mweusi alikisogeza kitanda ili afagie, aliona shimo dogo.

Alijiuliza, "Nani alichimba shimo hili?"




Aliwaita Paka wenzake kuja kuangalia shimo lile.

Bila shaka mwizi wa mkate wetu hupita kwenye shimo hili.

“Sasa tutamkamata tu,” walisema wote kwa pamoja.

Siku iliyofuata jioni,
Paka wa bluu alipika mikate mitatu mitamu.
Badala ya kwenda kulala walijificha.





Usiku sana, Panya mkubwa wa rangi ya manjano alijitokeza. Aliuendea mkate.

Paka walijitokeza kwa pamoja, “Tumekupata!” walisema paka.
“Turudishie mkate wetu!” Paka walimuweka juu ya meza ili awajibu vizuri. Panya alitoa macho kwa hofu.





“Kama nikiwapa mkate huu, watoto wangu watakufa kwa njaa.” Alisema Panya. “Mimi ni mgonjwa sana siwezi kwenda mbali kutafuta chakula.”

Paka waliwaangalia watoto
wa Panya walivyokonda.





Siku iliyofuata, Paka wa bluu alipika mikate mikubwa ya kuwatosha wote. Walikula kwa pamoja na kufurahia.